

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 1 AGOSTI 2018

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika **Jumatano, Tarehe 1 Agosti 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchini, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Julai 2018. Kwa mwezi Agosti 2018, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 25/lita (sawa na asilimia 1.04) na Shilingi 38/lita (sawa na asilimia 1.62), sawia, wakati bei za rejareja za Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 78/lita (sawa na asilimia 3.58). Vilevile, ukilinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli nazo zimepungua kama ifuatavyo; Shilingi 24.98/lita (sawa na asilimia 1.09) na Shilingi 37.68/lita (sawa na asilimia 1.71), sawia, wakati bei za Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 78.26/lita (sawa na asilimia 3.78). Mabadiliko haya ya bei yanatokana na kupungua kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premium*) na mabadiliko ya bei za mafuta kwenye soko la dunia kama ifuatavyo:
 - i. katika kukokotoa bei za mafuta za mwezi Agosti 2018, shehena nne za mafuta ya Petroli na Dizeli kati ya tano zilizopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam mwezi Julai 2018 zilinunuliwa kwa bei ya mafuta ya soko la dunia ya mwezi Juni 2018, ambapo bei hiyo ni pungufu ukilinganisha na bei ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018 iliyotumika kukokotoa bei za mwezi Julai 2018.
 - ii. katika kukokotoa bei za mafuta za mwezi Agosti 2018, shehena ya Mafuta ya Taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Dar es Salaam mwezi Julai 2018 ilinunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018. Ifahamike kuwa, shehena ya mwisho ya Mafuta ya Taa kupokelewa katika bandari ya Dar es Salaam ilikuwa mwezi Mei 2018 ikiwa imenunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Aprili 2018 ambayo ni pungufu ya bei ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018.
- (b) Kwakuwa hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Julai 2018, bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kaskazini zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Julai 2018. Shehena ya mwisho ya mafuta ilipokelewa katika bandari ya Tanga mwezi Mei 2018 ikiwa imenunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Machi 2018. Vilevile, kutokana na ghala la kuhifadhi mafuta lililopo Tanga kuishiwa Mafuta ya Taa, wamiliki wa vituo vya mafuta katika Mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitatokana na gharama za mafuta hayo yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.
- (c) Vilevile, kwakuwa hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Mtwara katika mwezi wa Julai 2018, bei za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Mtwara zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Julai 2018. Shehena ya mwisho ya mafuta ilipokelewa katika bandari ya Mtwara mwezi Juni 2018 ikiwa imenunuliwa kwa bei

ya soko la dunia ya mwezi Mei 2018. Kutokana na kuwepo kwa mafuta mengi katika maghala ya kuhifadhi mafuta Mtwara, bei za mafuta kwa mkoa wa Ruvuma zimekokotolewa kutokana na gharama za mafuta kutoka Mtwara. Hivyo, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Mtwara. Kwakuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zitatakana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi Mtwara na Ruvuma.

- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za kiganjani kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 269/2018 la mwezi Juni 2018**.
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---------------------------|-----------------------|----------------------|-----------------------------|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| Dar es Salaam | 2,384 | 2,292 | 2,271 |
| Arusha | 2,291 | 2,225 | 2,355 |
| Arumeru (Usa West) | 2,291 | 2,225 | 2,355 |
| Karatu | 2,309 | 2,243 | 2,373 |

| | | | |
|----------------------------|--------------|--------------|--------------|
| Longido | 2,302 | 2,236 | 2,366 |
| Monduli | 2,296 | 2,230 | 2,360 |
| Monduli-Makuyuni | 2,301 | 2,235 | 2,365 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,375 | 2,309 | 2,446 |
| Pwani (Kibaha) | 2,388 | 2,296 | 2,275 |
| Bagamoyo | 2,395 | 2,303 | 2,282 |
| Chalinze Junction | 2,398 | 2,306 | 2,285 |
| Chalinze (Msata) | 2,402 | 2,310 | 2,289 |
| Kibiti | 2,404 | 2,312 | 2,291 |
| Kisarawe | 2,391 | 2,299 | 2,278 |
| Mkuranga | 2,393 | 2,301 | 2,280 |
| Rufiji | 2,411 | 2,319 | 2,298 |
| Dodoma | 2,442 | 2,350 | 2,329 |
| Bahi | 2,450 | 2,358 | 2,337 |
| Chamwino | 2,438 | 2,346 | 2,325 |
| Chemba | 2,469 | 2,377 | 2,356 |
| Kondoa | 2,475 | 2,383 | 2,362 |
| Kongwa | 2,440 | 2,348 | 2,327 |
| Mpwapwa | 2,444 | 2,352 | 2,331 |
| Mtera (Makatopora) | 2,461 | 2,369 | 2,348 |
| Geita | 2,549 | 2,457 | 2,436 |
| Bukombe | 2,538 | 2,446 | 2,425 |
| Chato | 2,570 | 2,478 | 2,457 |
| Mbogwe | 2,587 | 2,495 | 2,474 |
| Nyang'hwale | 2,564 | 2,472 | 2,451 |
| Iringa | 2,448 | 2,356 | 2,335 |
| Ismani | 2,453 | 2,361 | 2,340 |
| Kilolo | 2,452 | 2,360 | 2,339 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,458 | 2,366 | 2,345 |
| Kagera (Bukoba) | 2,599 | 2,507 | 2,486 |
| Biharamulo | 2,573 | 2,481 | 2,460 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,616 | 2,524 | 2,503 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,621 | 2,529 | 2,508 |
| Muleba | 2,599 | 2,507 | 2,486 |
| Ngara | 2,587 | 2,495 | 2,474 |
| Misenyi | 2,608 | 2,516 | 2,495 |
| Katavi (Mpanda) | 2,592 | 2,500 | 2,479 |
| Mlele (Inyonga) | 2,573 | 2,481 | 2,460 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,584 | 2,492 | 2,471 |
| Kigoma | 2,615 | 2,523 | 2,502 |
| Uvinza (Lugufu) | 2,627 | 2,535 | 2,514 |
| Buhigwe | 2,604 | 2,512 | 2,491 |
| Kakonko | 2,572 | 2,480 | 2,459 |
| Kasulu | 2,601 | 2,509 | 2,488 |
| Kibondo | 2,579 | 2,487 | 2,466 |
| Kilimanjaro (Moshi) | 2,280 | 2,214 | 2,344 |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,283 | 2,217 | 2,348 |
| Mwanga | 2,273 | 2,207 | 2,338 |

| | | | |
|----------------------------|--------------|--------------|--------------|
| Rombo (Mkuu) | 2,297 | 2,231 | 2,365 |
| Same | 2,267 | 2,200 | 2,331 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,287 | 2,221 | 2,351 |
| Lindi | 2,443 | 2,350 | 2,330 |
| Lindi-Mtama | 2,461 | 2,369 | 2,348 |
| Kilwa Masoko | 2,417 | 2,325 | 2,305 |
| Liwale | 2,463 | 2,371 | 2,351 |
| Nachingwea | 2,472 | 2,380 | 2,359 |
| Ruangwa | 2,473 | 2,381 | 2,360 |
| Manyara (Babati) | 2,325 | 2,259 | 2,393 |
| Hanang (Katesh) | 2,335 | 2,269 | 2,404 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,340 | 2,274 | 2,404 |
| Mbulu | 2,337 | 2,271 | 2,406 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,357 | 2,291 | 2,425 |
| Mara (Musoma) | 2,562 | 2,470 | 2,449 |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,603 | 2,511 | 2,490 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,571 | 2,479 | 2,458 |
| Rorya (Shirati) | 2,606 | 2,514 | 2,493 |
| Bunda | 2,553 | 2,461 | 2,440 |
| Butiama | 2,559 | 2,467 | 2,446 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,608 | 2,516 | 2,495 |
| Tarime | 2,573 | 2,481 | 2,460 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,578 | 2,486 | 2,465 |
| Mbeya | 2,491 | 2,399 | 2,378 |
| Chunya | 2,500 | 2,408 | 2,387 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,515 | 2,422 | 2,402 |
| Kyela | 2,507 | 2,414 | 2,394 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,475 | 2,383 | 2,362 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,500 | 2,408 | 2,387 |
| Morogoro | 2,409 | 2,317 | 2,296 |
| Mikumi | 2,424 | 2,332 | 2,311 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,446 | 2,354 | 2,334 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,469 | 2,377 | 2,356 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,458 | 2,366 | 2,345 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,457 | 2,365 | 2,344 |
| Malinyi | 2,467 | 2,375 | 2,354 |
| Kilosa | 2,427 | 2,335 | 2,314 |
| Gairo | 2,427 | 2,335 | 2,314 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,419 | 2,327 | 2,306 |
| Turiani | 2,434 | 2,342 | 2,321 |
| Mtwara | 2,387 | 2,360 | 2,343 |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,429 | 2,402 | 2,392 |
| Masasi | 2,409 | 2,382 | 2,369 |
| Newala | 2,414 | 2,387 | 2,375 |
| Tandahimba | 2,407 | 2,380 | 2,368 |
| Nanyamba | 2,407 | 2,380 | 2,368 |
| Mwanza | 2,534 | 2,442 | 2,421 |
| Kwimba | 2,552 | 2,460 | 2,439 |

| | | | |
|-----------------------------|--------------|--------------|--------------|
| Magu | 2,542 | 2,450 | 2,429 |
| Misungwi | 2,528 | 2,436 | 2,415 |
| Sengerema | 2,566 | 2,474 | 2,453 |
| Ukerewe | 2,593 | 2,501 | 2,480 |
| Njombe | 2,476 | 2,384 | 2,363 |
| Njombe (Kidegembye) | 2,497 | 2,405 | 2,384 |
| Ludewa | 2,514 | 2,422 | 2,401 |
| Makambako | 2,468 | 2,376 | 2,355 |
| Makete | 2,507 | 2,415 | 2,394 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,474 | 2,382 | 2,361 |
| Rukwa (Sumbawanga) | 2,557 | 2,465 | 2,444 |
| Sumbawanga Rural (Mtownisa) | 2,557 | 2,465 | 2,444 |
| Kalambo (Matai) | 2,564 | 2,472 | 2,451 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,570 | 2,478 | 2,457 |
| Ruvuma (Songea) | 2,472 | 2,445 | 2,394 |
| Mbinga | 2,485 | 2,458 | 2,428 |
| Namtumbo | 2,463 | 2,436 | 2,423 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,510 | 2,483 | 2,430 |
| Tunduru | 2,438 | 2,411 | 2,453 |
| Shinyanga | 2,513 | 2,420 | 2,400 |
| Kahama | 2,526 | 2,434 | 2,413 |
| Kishapu | 2,541 | 2,449 | 2,428 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,544 | 2,452 | 2,431 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,554 | 2,462 | 2,441 |
| Busega (Nyashimo) | 2,547 | 2,455 | 2,434 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,557 | 2,465 | 2,444 |
| Maswa | 2,545 | 2,453 | 2,433 |
| Meatu (Mwanzuhi) | 2,553 | 2,460 | 2,440 |
| Singida | 2,474 | 2,382 | 2,361 |
| Iramba | 2,486 | 2,394 | 2,374 |
| Manyoni | 2,459 | 2,367 | 2,346 |
| Ikungi | 2,470 | 2,378 | 2,357 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,499 | 2,407 | 2,386 |
| Songwe (Vwawa) | 2,500 | 2,408 | 2,387 |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,507 | 2,415 | 2,394 |
| Ileje | 2,504 | 2,412 | 2,391 |
| Momba (Chitete) | 2,509 | 2,417 | 2,396 |
| Tunduma | 2,504 | 2,412 | 2,391 |
| Tabora | 2,538 | 2,446 | 2,425 |
| Igunga | 2,492 | 2,400 | 2,379 |
| Kaliua | 2,557 | 2,465 | 2,444 |
| Ulyankulu | 2,551 | 2,459 | 2,438 |
| Nzega | 2,502 | 2,410 | 2,389 |
| Sikonge | 2,550 | 2,458 | 2,437 |
| Urambo | 2,551 | 2,459 | 2,438 |
| Uyui | 2,539 | 2,447 | 2,426 |
| Tanga | 2,234 | 2,168 | 2,317 |
| Handeni | 2,255 | 2,188 | 2,296 |

| | | | |
|------------------|-------|-------|-------|
| Kilindi | 2,270 | 2,203 | 2,331 |
| Korogwe | 2,246 | 2,180 | 2,310 |
| Lushoto | 2,255 | 2,189 | 2,320 |
| Mkinga (Maramba) | 2,241 | 2,175 | 2,331 |
| Muheza | 2,239 | 2,173 | 2,317 |
| Pangani | 2,241 | 2,175 | 2,323 |

B: BEI ZA JUMLA

| Bei za Jumla - DSM | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|--------------------|--------------------|-------------------|--------------------------|
| Bei Kikomo | 2,259.15 | 2,166.99 | 2,146.78 |

| Bei za Jumla - TANGA | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|----------------------|--------------------|-------------------|--------------------------|
| Bei Kikomo | 2,109.92 | 2,043.69 | --- |

| Bei za Jumla - MTWARA | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|-----------------------|--------------------|-------------------|--------------------------|
| Bei Kikomo | 2,262.35 | 2,235.07 | --- |

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA